

**HOTUBA YA MTENDAJI MKUU WA TAASISI YA SANAA NA
UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa) KATIKA UFUNGUZI WA TAMASHA
LA 37 LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
TAREHE 20 OKTOBA, 2018**

- Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dr. Harrson George Mwakyembe (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.
- Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Mhe. Zainabu Kawawa
- Mbunge, Jimbo la Bagamoyo, Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb.)
- Katibu Tawala Wilaya ya Bagamoyo, Mhe. Hamza Amri Athumani
- Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Bagamoyo.
- Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Bibi Leah Kihimbi
- Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.
- Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Mhe. Habbi Gunze
- Mwenyekiti wa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Prof Frowin Paul Nyoni
- Waheshimiwa Mabalizi wa Nchi mbali mbali waliofika leo.
- Mkurugenzi wa Utangazaji TCRA, Bw. Frederick Ntobi
- Mkurugenzi Mkuu - TBC, Dr. Ayub Rioba
- Katibu wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Bw. Godfrey Mngereza
- Katibu wa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Bibi Joyce Fisso
- Mkuu wa Idara ya Sanaa Bunifu, CKD - Dr Kedmond Mapana
- Wafadhili wetu wote
- Marais wote wa Mashirikisho ya Sanaa Tanzania
- Waheshimiwa Viongozi Mbalimbali,
- Wahitimu, Wafanyakazi na Wanafunzi wa TaSUBa
- Wasanii wote,
- Wadau wa sanaa,
- Mabibi na Mabwana.

Habari ya mchana,

Mgeni rasmi,

Nianze kwa kutoa shukrani zetu za dhati kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi katika tukio hili mahsusi la ufunguzi wa Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni lenye kauli mbiyu - *“Sanaa Na Utamaduni Katika Kukuza Uzalendo”*.

Mgeni rasmi,

Kama wengi tunavyofahamu, mwaka huu Tamasha hili la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo linatimiza miaka 37 tangu lilipoasisiwa mwaka 1981. Umri wa miaka 37 wa Tamasha hili si kidogo; huu ni umri wa mtu mziama. Hivyo, pamoja na changamoto nyingi zilizopo, kwa hakika sisi Taasisi pamoja na wadau wetu wote tunajivunia mafaniko makubwa tuliyoyapta ndani ya miongo karibia mine ya uwepo wa Tamasha hili.

Mgeni rasmi,

Kama ada, Tamasha hili la 37 la limevutia ushiriki wa vikundi vingi vya sanaa vya hapa nchini ikiwa ni pamoja maonyesho yatakayo oneshwa na wanafunzi na wafanyakazi wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Tunawashukuru sana wasanii wote mnaoshiriki na wale ambao mara hii hawakufika hapa kwa kuendelea kutumia Tamasha hili kuonyesha kazi zenu, kujifunza na kutoa fursa ya wasanii wengine kujifunza kutoka kwenu.

Mgeni rasmi,

Kwa heshima na taadhima niwashukuru viongozi wote wa serikali, mashirika, vyama vya siasa, wakazi wote wa mji na wilaya yetu ya Bagamoyo na majirani zetu wote, kwa misaada na ushirikiano mkubwa mnaotupatia si katika Tamasha hili tu bali kwenye shughuli zote ambazo Taasisi imekuwa ikizifanya. Asanteni sana.

Mgeni rasmi,

Kwa dhati kabisa niwashukuru wasanii wote waliopo hapa na wale ambao wataendelea kuungana nasi kwa wiki nzima ya Tamasha hili. Aidha, kwa niaba ya Taasisi nawashukuru na kuwakaribisha wageni wetu wote mlioitikia mwaliko wetu. Kwa hakika bila ninyi Tamasha hili haliwezi kuwa tamasha.

Aidha, nitoe shukurani zetu kwa uongozi wa juu wa Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Waheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Watumishi wote wa Wizara kwa ushauri na ushirikiano mkubwa mnaotupatia.

Pia nikishukuru kitengo cha Maonyesho na Tamasha - TaSUBa, Kamati zote za Tamasha na Wanafanyakazi wote wa TaSUBa kwa kazi kubwa mliyofanya katika kuandaa Tamasha hili. Bila kuwasahau wanachuo waliopo sasa na wale waliopita kwa ushiriki wao walidhawa kwenye Tamasha hili.

Mgeni rasmi,

Nichukue fursa hii kuwashukuru wadhamini wote wa Tamasha hili. Wadhamini hao ni pamoja na:- CRDB, Embassy of the Federal Republic of Germany, Bagamoyo Friendship Society, TBC, Travelers Lodge, Millennium Sea Breeze Resort, Country Club, Funky Squid Beach Hotel, Michuzo Blog, Mlimani TV, Mlimani Radio, Printing and Signs Solutions, Dept. of Creative Arts - University of Dar Es Salaam, Esther Decorations and Printing, Alpha Lodge, New Habari (2006) Ltd, Sherehe Arts Association (SAA), Lowland View Resort, Sokaextra Blog, Pata Ufahamu Blog, Mwanaharaka Mzalendo Blog, Raia Mwema Company Ltd, Trust Signs, Nashe's Café, Social Security Regulatory Authority (SSRA), Vijana Vipaji Foundation (VVVF), Art Moves Africa (AMA), Vema Lodge, Mak's Lodge, Bagamoyo Monie Hotel, Town Lodge, Bakhresa Food Products, Suma JKT, Tanzania Federation Of Crafts And Arts (TAFCA), Tanzania National Parks (TANAPA) - Saadani National Part, TACIP, Uhuru Peak Water, Data Vision, Acto Light, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Daily News, Habari Leo, Tan-trade, na vikundi mbalimbali vilivyoweza kujigharimia na kushiriki Tamasha.

Nimalizie kwa kukushukuru kwa mara nyingine tena kwa kukubali mwaliko wetu wa kuja kufungua Tamasha hili.

Asanteni sana kwa kunisikiliza